

Jina la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo lihimidiwe daima, karibu tujifunze Biblia Neno la Mungu wetu lililo taa ya miguu yetu na Mwanga wa njia yetu (**Zab.119:105**).

Maandiko yanatuonyesha kuwa si lazima watu wote wanene kwa lugha (*1Wakorintho 12:30 na 14:23*), kana kwamba ndio uthibitisho pekee wa mtu kuwa wa kiroho...lakini pia kuna faida kubwa ya kunena kwa lugha ikiwa mtu atajaliwa hilo.

Na pia kunena kwa lugha si jambo ambalo mtu anaweza kuamua, kwamba sasa naanza kunena, la! Kunena kwa lugha ni msukumo ambao Roho Mtakatifu anaushusha ndani ya mtu pasipo mtu kutaka au kupanga!.. Ni kama mtu anavyopokea unabii, au anavyopokea ndoto au maono.. hakuna mtu anayeweza kupanga unabii au maono au ndoto (*labda awe nabii wa uongo*)!.. kwani mambo hayo yanakuja tu yenyewe kutoka kwa Mungu, kwajinsi apendavyo Mungu... Na kunena kwa lugha ni hivyo hivyo, si lazima iwe kila siku au kila saa, bali ni wakati maalumu tu ambao Roho atalishusha jambo hilo ndani ya mtu.

Sasa zipo lugha za wanadamu, na vile vile za Malaika (*Soma 1Wakorintho 13:1*), Zozote kati ya hizo mtu aliyejazwa Roho anaweza kuzinena. Na zote zina faida katika kuzinena... Katika kunena lugha za wanadamu ni pale ambapo mtu haijui lugha Fulani ya jamii fulani ya

watu, lakini ghafla anajikuta anaanza kuizungumza ile lugha vizuri sana.. Vile vile katika kunena lugha za malaika, ni pale ambapo anajikuta anazungumza lugha ambayo ni mpya kabisa isiyotumiwa na wanadamu mahali popote.

Na maneno anayoyazungumza yanakuwa aidha ni maneno ya unabii, au maonyo au ya kumsifu Mungu.. kwahiyo kama ni ujumbe kwa kanisa ni lazima awepo mfasiri..

Vile vile kama ni lugha Mpya inayozungumzwa, maana yake ambayo haitumiki na jamii yoyote ya wanadamu, na ni ujumbe kwa kanisa, basi anahitajika pia mfasiri, lakini kama mtu yupo katika maombi yake binafsi na lugha hiyo ikamjia ndani yake, basi hapo hahitaji mfasiri bali anakuwa ananena maneno ya siri na Mungu wake.

Na leo tutaangalia faida moja kubwa ya kunena lugha mpya, uwapo wewe binafsi katika maombi yako ya faragha.

MAZUNGUMZA YAKO YANAKUWA NI YA SIRI.

Hii ndio faida kuu na ya kwanza. Kikawaida mazungumzo ya siri yanakuwa na upinzani mchache kuliko mazungumzo ya wazi!.. na njia mojawapo ya kuficha mazungumzo ni kutumia lugha nyingine!..

Kwamfano utaona Waarabu wawili, au Wachaga wawili, au wamasai wawili, au wasukuma wawili, wanapokutana mahali Fulani ili waongee kwa uhuru zaidi utaona wanatumia lugha zao za asili , lengo ni kuficha mazungumzo na pia kuzungumza mambo yao yale mambo ya ndani kwa uhuru zaidi.. watu walio kando kando inakuwa ngumu kuelewa na hivyo wazungumzaji wanakuwa wamefunga milango mingi.

Na sisi tunapozungumza na Mungu wetu, **KUNA WAKATI TUNAHITAJI USIRI**.. Maneno yetu tunayoyazungumza si lazima yaeleweke na watu wa kando yetu au na mapepo katika ulimwengu wa roho. Ili kuzuia vita visivyokuwa na msingi.

Shetani asipoelewa kile tunachoomba kwa Mungu, inamwia vigumu kwake kupanga mashambulizi, kwasababu hajui ni nini tunamwomba Mungu kwa wakati huo, hivyo anabaki tu hapo katikati, lakini akisikia unamwomba Mungu akupe Amani, au akupe riziki Fulani, tayari na yeye kashajua ni eneo gani aende kukupiga vita ili usipokee kile ulichomwomba Mungu. Ndio maana Mtume Paulo kwa ufunuo wa roho aliliona hilo na akawaandikia watakatifu..

1Wakorintho 14:2 “Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu,

bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake”.

Hivyo usijizue kunena kwa lugha kama umejaliwa hilo.. itakusaidia kuzuia vita vingi katika ulimwengu wa mwili na wa roho.

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Je kunena kwa Lugha mpya kukoje?

JE! UMEPOKEA KWELI ROHO MTAKATIFU?

SEMA KWA LUGHA NYINGINE.

IJUE FAIDA YA KUNENA KWA LUGHA MPYA!

MBINGU MPYA NA NCHI MPYA. (Sehemu ya 1)

USHIRIKA WA ROHO MTAKATIFU UKAE NANYI NYOTE.

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp